**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
**OFISI YA RAIS,**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.**
**SHULE YA SEKONDARI**

# MTIHANI WA KIDATO CHA KWANZA
## KISWAHILI

MUDA: MASAA 2:30 2024

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, na C zenye jumla ya maswali kumi (10).
2. Jibu maswali yote katika sehemu A, B na C.
3. Sehemu **A** ina alama **15,** sehemu **B** alama **70** na shemu **C** ina alama **15.**
4. Zingatia maelezo ya **kila sehemu** na ya **kila swali.**
5. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

| KWA MATUMIZI YA MTAHINI | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **ALAMA** | **SAINI YA MTAHINI** |
| 1 | | |
| **2** | | |
| **3** | | |
| **4** | | |
| **5** | | |
| **6** | | |
| **7** | | |
| **8** | | |
| **9** | | |
| **10** | | |
| **JUMLA YA ALAMA** | | |

## SEHEMU A (alama 15)

**Jibu maswali yote katika sehemu hii**

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x) kisha andika herufi ya jibu katika karatasi ya kujibia.

i. Mama yake asha amemmunulia mwanae Gari jipya **japokuwa** halipendi kabisa.Je katika sentensi hiyo neno japokuwa limetumika kama aina gani ya neno.

A. Kitenzi
B. Nomino
C. Kielezi
D. Kihusishi
E. Kiunganishi

ii. Waswahili husema kata pua uunge wajihi.Je neno wajihi katika methali hiyo linamaanisha nini?

A. Mishipa
B. Uchonge pua
C. Sura
D. Macho
E. Meno

iii. Kiswahili kina utajiri wa misamiati mbalimbali.Je mtu anaefanya kazi ya kufua vyuma huitwaje?

A. Topasi
B. Mhunzi
C. Mlonzi
D. Vyumavu
E. Mtozi

iv. Ufasaha wa lugha hutawaliwa na mambo makuu manne ndani yake ambayo ni fonolojia, mofoloji,sintaksia.Je jambo la nne linalokamilisha mambo hayo ni lipi kati ya haya yafuatayo;

A. Matamshi
B. Maumbo ya maneno
C. Miundo ya tungo
D. Maana za tungo
E. Mitindo ya maneno

v. Seypalm ni mwanafunzi katika shule ya mtakuja, alisema " fani ni chombo Cha kuelezea maudhui kwa namna inayovutia". Kutokana na ulivyosema mada ya fasihi kidato Cha kwanza, unafikili fani katika fasihi ni nini

A. Umbo la ndani la kazi ya fasihi
B. Mpangilio wa kazi ya fasihi
C. Umbo la nje la kazi ya fasihi
D. Mandhari ya kazi ya kazi ya fasihi
E. Ni uzuri uliosanifishwa

vi. Sauti za lugha ambazo zina maana na ambazo zimekubaliwa na watu wa lugha Fulani ili zitumike katika mawasiliano huwa zinaitwa;

A. Matamshi
B. Silabi
C. Fonimu
D. Lafudhi
E. Mofimu

vii. Suzuki ana mkono wa birika.Je Katika sentensi hiyo,maana ya nahau hiyo inaweza kuwa;

A. Anamkono uliopinda
B. Mwizi
C. Mbahili
D. Mchoyo
E. Anasaidia watu

viii. Miongoni mwa jambo linaloipa uhai fasihi simulizi ni ushirikishwaji wa hadhira, unahisi ni jambo gani lingine linaloweza kuipa uhai kazi ya fasihi simulizi.

A. Uibuaji wa hisia
B. Kutokuwa na gharama
C. Haibagui hadhira
D. Kuhifadhiwa kichwani
E. Kuwa na tanzu chache.

ix. Mwalimu wetu wa darasa amemzawadia mwanafunzi aliyefanya vizuri katika somo la kiswahili kamusi yenye lugha mbili ambazo ni Kiswahili na kiingereza.Je kamusi yenye lugha mbili katika muktadha wa kiswahili huwa inaitwa:

A. Kamusi Mahuluti
B. Kamusi Thaniya

C. Kamusi wahidiya
D. Kamusi Maulama
E. Kamusi tirigivyongo

x. Fungu la sauti zinazotokea katikati au mwishoni mwa kila mshororo wa ubeti wa shairi huitwaje?
A. Mstari
B. Vina
C. Silabi
D. Mizani.
E. Urari

| i. | ii. | iii. | iv. | v. | vi. | vii. | viii. | ix. | x. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

2. Oanisha maelezo yaliyopo katika orodha A na kuchagua istilahi husika katika Orodha B ili kukamilisha maana. kisha andika herufi husika katika karatasi ya majibu.

| **ORODHA A** | **ORODHA B** |
|---|---|
| i. Hutawaliwa na malumbano yenye kusudi la kutoa ujumbe maalumu. | A. Maghani |
| ii. Mpangilio maalumu wenye mahadhi ya kushuka na kupanda kwa sauti. | B. Maigizo |
| iii. Husemwa au hughanwa kwa sauti Fulani ambayo ipo katika uzungumzaji na uimbaji. | C. Mashairi |
| iv. Ni mpangilio maalumu wa maneno wenye ruwaza mahususi ya silabi, lugha ya mkato na ya kinudhumu | D. Ngonjera |
| v. Huwa na maudhui ya kihistoria yenye kuadilisha au kuadibu katika muundo wa usimulizi. | E. Utenzi |
| | F. Tendi |
| | G. Nyimbo |

| **ORODHA A** | **i.___** | **ii.___** | **iii.___** | **iv.___** | **v.___** |
|---|---|---|---|---|---|
| **ORODHA B** | | | | | |

## SEHEMU B. (Alama 70)
### Jibu maswali yote

3. Mara baada ya kujifunza aina za maneno, Mwalimu aliwaita wanafunzi ubaoni watunge na kuandika sentensi tano zenye viunganishi vya sababu tofauti tofauti.Ukiwa wewe ni miongoni mwa wanafunzi hao tunga sentensi tano zenye viunganishi vya sababu kisha vibainishe kwa kuvipigia mstari.
   i. ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   ii. ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   iii. ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   iv. ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   v. ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………

4. Waswahili huweza kutoa dhana tofauti tofauti kuhusu lugha, Ukiwa kama mjuzi wa lugha ya kiswahili bainisha mambo makuu Matano ya kuzingatia pindi unapotoa maana ya lugha.
   i. ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………
   ii. ……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………

iii. ………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

iv. ………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

v. ………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

5. Kamusi huwa na taarifa mbalimbali zinazopatikana ndani yake, miongoni mwa taarifa hizo ni michoro na picha mbalimbali.Elezea kwa hoja tano faida za picha na michoro katika kamusi

i. ………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

ii. ………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

iii. ………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

iv. ………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

v. ………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

6. Fasihi simulizi imegawanyika katika tanzu kuu nne ambazo ni Hadithi, semi, ushauiri na Maigizo na ndani ya tanzu hizo kuna vipera ndani yake.Ukiwa kama mwanafasihi chunguza jedwali ulilopewa kisha bainisha vipera vitano vilivyojitokeza ndani ya jedwali hili kisha vizungushie na uvibainishe hapo chini.

| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **E** | **R** | **T** | **Y** | **U** | **I** | **O** | **G** | **D** | **S** | **O** | **D** | **A** | **D** | **A** | **M** | **U** | **D** | **F** | **J** |
| **R** | **G** | **U** | **I** | **O** | **V** | **M** | **I** | **V** | **I** | **J** | **A** | **S** | **V** | **N** | **K** | **O** | **L** | **P** | **J** |
| **W** | **U** | **K** | **O** | **L** | **P** | **V** | **I** | **C** | **A** | **D** | **R** | **T** | **Y** | **H** | **K** | **L** | **U** | **G** | **H** |
| **R** | **R** | **H** | **Q** | **G** | **H** | **J** | **U** | **Z** | **W** | **E** | **R** | **T** | **H** | **Q** | **A** | **R** | **R** | **Q** | **Q** |
| **G** | **Y** | **C** | **A** | **W** | **V** | **B** | **N** | **M** | **U** | **N** | **G** | **O** | **N** | **W** | **P** | **Y** | **T** | **R** | **W** |
| **Y** | **M** | **R** | **V** | **F** | **G** | **H** | **J** | **N** | **I** | **N** | **J** | **A** | **J** | **D** | **L** | **U** | **G** | **T** | **E** |
| **H** | **R** | **A** | **T** | **Z** | **C** | **V** | **N** | **H** | **E** | **T** | **G** | **O** | **F** | **K** | **M** | **K** | **H** | **Y** | **R** |
| **J** | **G** | **Q** | **G** | **Q** | **W** | **E** | **I** | **G** | **H** | **O** | **Z** | **U** | **T** | **L** | **K** | **L** | **J** | **U** | **T** |
| **I** | **H** | **D** | **T** | **H** | **Y** | **R** | **U** | **U** | **S** | **W** | **E** | **R** | **R** | **O** | **I** | **P** | **K** | **J** | **H** |
| **K** | **U** | **H** | **F** | **W** | **A** | **N** | **G** | **N** | **G** | **G** | **H** | **J** | **E** | **P** | **U** | **O** | **I** | **M** | **M** |
| **L** | **K** | **U** | **G** | **T** | **B** | **N** | **B** | **N** | **B** | **M** | **D** | **R** | **W** | **U** | **J** | **I** | **O** | **K** | **K** |
| **O** | **P** | **K** | **V** | **R** | **T** | **Y** | **I** | **N** | **Z** | **F** | **H** | **J** | **D** | **N** | **N** | **U** | **L** | **I** | **L** |
| **E** | **L** | **O** | **E** | **W** | **R** | **A** | **Q** | **W** | **P** | **A** | **E** | **U** | **S** | **F** | **H** | **Y** | **M** | **O** | **O** |
| **L** | **M** | **L** | **R** | **S** | **Q** | **W** | **A** | **E** | **O** | **E** | **T** | **J** | **F** | **T** | **Y** | **T** | **N** | **P** | **P** |
| **U** | **N** | **V** | **F** | **A** | **Y** | **R** | **W** | **T** | **T** | **U** | **Y** | **M** | **G** | **H** | **A** | **R** | **B** | **D** | **Y** |
| **G** | **C** | **N** | **G** | **D** | **U** | **T** | **R** | **U** | **K** | **K** | **U** | **K** | **G** | **G** | **T** | **E** | **V** | **F** | **G** |
| **H** | **S** | **M** | **H** | **F** | **I** | **I** | **F** | **J** | **M** | **I** | **I** | **K** | **I** | **H** | **G** | **W** | **C** | **T** | **D** |
| **A** | **W** | **J** | **U** | **G** | **K** | **K** | **V** | **K** | **J** | **K** | **K** | **V** | **Y** | **K** | **B** | **Q** | **X** | **G** | **F** |
| **E** | **E** | **A** | **J** | **V** | **H** | **L** | **B** | **I** | **H** | **K** | **I** | **W** | **H** | **L** | **H** | **A** | **Z** | **H** | **R** |
| **B** | **R** | **W** | **K** | **H** | **N** | **M** | **M** | **O** | **N** | **M** | **L** | **E** | **N** | **M** | **N** | **A** | **A** | **N** | **T** |

i. ………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

ii. ………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

iii. ……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
iv. ……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
v. ……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

7. Fafanua istilahi zifuatazo kama zinavyotumika kati mawasiliano:-
   a) Wakaa……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   b) Shadda……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   c) Kidatu……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   d) Kiimbo……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   e) Fonimu……………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………

8. Fasihi ni tawi la sanaa linalotumia lugha ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira, Matawi mengine ya sanaa ni kama vile ufinyanzi,ususi,useremala,uchongaji n.k.Ukiwa kama mwanafasihi elezea mambo Matano yanayotofautisha fasihi na matawi mengine ya sanaa.
   i. ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   ii. ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   iii. ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   iv. ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………
   v. ……………………………………………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………

9. Soma Habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata: -

   Kipindi cha kuanzia mwaka 1930 hadi 1938 kilikuwa muhimu sana kwa historia ya **usanifishaji** wa Kiswahili.Mambo mbalimbali yalifanyika ili kuhakikisha kuwa kinasitawi na kushamiri. Kuundwa kwa **kamati** maalumu ya kushughulikia lugha ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki, ilikuuwa hatua muhimu sana katika kukikuza na kukiendeleza Kiswahili.

   Kazi za kamati ya lugha ya Afrika Mashariki zilikuwa nyingi kama vile, kusanifisha otografia itakayotumika kwa watumiaji wote wa Kiswahili, kuandaa kamusi mbalimbali, kutoa **hamasa** kwa waandishi wachanga wanaotumia lugha ya Kiswahili katika kuandika kazi zao, kusahihisha lugha katika vitabu vilivyokuwa vinatumika kufundishia shuleni na kufanya tafiti mbalimbali za lugha ya kiswahili.

Kamati ya lugha ya Afrika Mashariki ilifanya kazi chini ya usimamizi wa utawala wa mwingereza. Kazi za kamati Zilipamba moto huku tafiti mbalimbali kuhusu lahaja za Kiswahili zikiendelea kufanyika. Tafiti hizo zilizaa matunda na hatimaye ikaonekana ni vizuri kuchagua lahaja moja na kuisanifisha ili iwe msingi wa kiswhili sanifu.

"Mungu hamtupi mja wake" **Sudi** iliangukia kwa lahaja ya kiunguja na ilichaguliwa kuwa lahaja ya Kiswahili sanifu.Watumiaji wa lahaja zingine walikuwa na **inda** baada ya lahaja ya kiunguja kutangazwa kuwa msingi wa usanifishaji wa Kiswahili. Kamati haikufanya ajizi, ilianza mara moja kazi ya kusanifisha lugha ya Kiswahili. Kiswahili sanifu tukitumiacho leo ni matunda ya kazi ya utawala wa waingereza katika usanifishaji wa lahaja ya kiunguja.

Kwa ujumla tunaweza kusema kati ya Wakoloni wote, Wakoloni wa Kiingereza ndio waliofanya kazi kubwa katika kukuza na kuiendeleza lugha ya Kiswahili. Kupitia **sera** na mfumo wa utawala wa wakati huo walifanya kazi kubwa kuhakikisha kuwa Kiswahili kinakuwa na kuenea katika nchi za Africa Mashariki.

Maswali:

(a) Toa maana ya maneno yafuatayo;

i. Kamati
ii. Sudi
iii. Inda
iv. Hamasa
v. Sera.

(b) Andika kichwa cha habari uliyoisoma kisichozidi maneno matatu.

(c) Mwandishi ana maana gani anaposema "Mungu hamtupi mja wake"?

(d) Fupisha habari uliyosoma kwa kutumia maneno sitini.

**SEHEMU 'C' Alama (15)**

10. Baba yako anaitwa Mwinjuma anayefanya kazi kama meneja katika kiwanda cha kusindika nyama S.L.P.3040 Singida.Wewe ukiwa kama mwanafunzi unayesoma katika shule ya sekondari Lukwaro S.l.P 6784 Kibaha, mwandikie barua kumtaarifu kuwa mmemaliza mitihani ya nusu muhula hivyo ajiandae kuja kukuchukua pindi shule itakavyofungwa.

………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...
………………………………………………………………………………………………...

……………………………………………………………………………………………………………...